Jarida la Shirika la Uboreshaji Miferej ya Asili na Uhifadhi wa Mazingira (TIP)

# Maendeleo ya TIP



## Je kikundi chako cha watumia maji ni imara?

1. Viongozi wanaojituma na waliochaguliwa kidemokrasia
2. Kila mwanachama anajua wajibu wake
3. Kinatunza kumbukumbu vizuri
4. Kinakutana mara kwa mara
5. Kimejenga mahusiano mazuri na wafanyabiashara na taasisi za mikopo
6. Kinatumia taarifa za masoko vizuri
7. Kinajifunza jinsi ya kufanya makubaliano na wanunuzi wa mazao
8. Kina akiba na michango
9. Kina katiba na sheria ndogo ndogo

## Siri ya kuimarika

Mvulana mmoja alikuwa akijaribu bila mafanikio kusogeza jiwe zito. Baba yake alikuwa amesimama pembeni yake na alimuuliza kwa nini hakutumia uwezo wake wote. Kijana alimueleza baba yake kuwa ndivyo alivyofanya. "Lakini kwanini hutaki msaada wangu? aliuliza baba. Watu wenye mafanikio hutumia uwezo wao wote kupata mafanikio. Hii humaanisha kwamba wanahitaji msaada pale unapohitajika tu. Kanuni ya uongozi ni kuwapa nafasi na kuwashirikisha wale unaowaongoza ili kuwafanya waelewe umuhimu wa mchango wao ili kufikia lengo. Jinsi unavyozidi kuwahusisha kushiriki ndivyo matokeo mazuri zaidi yanapotokea.

## Yaliyomo

TIP yaonngeza uwezo ........................ 2

Watu ................................................ 2

Maswali ya Ukimwi ............................ 2

Habari za wilayani ............................ 3

Shamba la mfano Moshi .................... 4

## Kukuza miradi endelevu kwa kutumia Wataalamu wenza

Madhumuni ya shirika la TIP ni kufanya kazi na vikundi vya wakulima vilivyo katika maeneo yenye umwagiliaji, kuviimarisha na kuviwezesha kujijengea maisha bora na endelevu. Njia madhubuti ya kuimarisha vikundi vya wakulima ni kutumia wataalamu wenza (VTs). Hawa wataalamu wenza, hupewa mafunzo maalumu ya uimarishaji wa vikundi na jinsia na mwangaza wa biashara, uhifadhi wa ardhi, uboreshaji wa mifumo ya umwagiliaji, na masoko. Wataalamu wenza husambaza taaluma waliyopata kwa wakulima wenzao katika kikundi na hata nje ya kikundi.

Likiwa kama shirika linalotoa huduma kwa wakulima wadogo, shirika huwaimarisha wakulima kwa njia ya hatua kwa hatua, inayowafanya kupata ufumbuzi wa matatizo yao. Shirika halitoweza kutoa huduma kwa kikundi kwa muda wote, baada ya muda fulani TIP hukiacha kikundi na kutoa huduma kwa kikundi kingine. Tafiti zinasema kwamba, kutoa msaada wa bure kwa muda mrefu matokeo yake ni kuwa tegemezi. Kwa upande wa TIP, ili miradi kuwa endelevu, wataalamu wenza ndio watakaokuwa na majukumu makubwa kwa wakati ujao. Mwezi Machi 2005, shirika lilitoa mafunzo kwa wataalamu wenza 17 wa wilaya ya Arumeru kwa muda wa wiki mbili. Mafunzo haya yataendeshwa kwa wilaya zote ambazo shirika linafanya kazi. Baada ya mafunzo, Wataalamu wenza watakuwa na jukumu la kusambaza na kufundisha wakulima wenzao katika kikundi na wasio katika kikundi.

## Masoko hubadilika kutokana na mahitaji ya jamii za mijini

Kulingana na taarifa ya makazi mijini ya Umoja wa mataifa, jamii zinaozishi vijijini katika nchi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara zinabadilika. Inategemewa ifikapo mwaka 2030, zaidi ya nusu ya watu wa eneo hili watakuwa wamehamia mijini. Uhamaji wa watu kutoka vijijini kwenda mijini humaanisha kwamba, kuna ongezeko kubwa la walaji wanaohitaji kununua vyakula kwa sababu hawawezi kuvizalisha wenyewe katika maeneo ya mijini. Kiwango cha ongezeko la watu Afrika ni asilimia 2 - 3 kwa mwaka. Ongezeko hili hutoa fursa kwa watu wa vijijini kuuza bidhaa zaidi.

Uhamiaji mijini una maana gani kwa wakulima wadogo na wajibu wao wa kuuza bidhaa masokoni? Vikundi vya wakulima vinatakiwa kutafuta mbinu bunifu za kutumia nguvukazi zao, rasilimali na ustadi wao kutumia vizuri nafasi za masoko mapya. Mfano mzuri ni wakulima wa Mamba Myamba kutoka wilaya ya Same, wanauza tangawizi Dar es Salaam na Zanzibar. Bei kwa mwaka 2004 ilikuwa shilingi za Kitanzania 250 kwa kilo. Wakulima wadogo wanatakiwa kujua soko, kujiunga na kuwa katika vikundi, kujua na kutumia mikakati mipya, kutafuta mbinu za kufanya bidhaa zao kuwa shindani, kuongeza ubora wa bidhaa zao

*Inaendelea Uk 2*

## Tanzia

Aliyekuwa mmojawapo wa waasisi wa Programu ya TIP miaka ya 1980, Bw. Raphaeli Burra, alifariki dunia mnamo tarehe 20/4/2005. Mafanikio ya kiutendaji ya programu ya TIP chini ya uangalizi wa Burra, yaliwezesha kupata tuzo kutoka Uholanzi ya Uendelezi wa Mazingira mwaka 1991. Aliondoka katika programu ya TIP mwaka 1998 kwenda kusoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Baadaye alijiunga na shirika lisilo la kiserika liitwalo PAMOJA. Raphaeli Burra atakumbukwa kwa uaminifu wake, utendaji mzuri wa kazi na mapenzi kwa kazi yake. Mungu ailaze pema roho ya marehemu Raphaeli Burra.



Bw. Raphael Burra (kushoto) akipokea tuzo ya Uholanzi ya Kuendeleza Mazingira.



**Kidokezo cha Afya cha Tangawizi**

Tangawizi ina madini kalshiam, fosforasi, chuma, vitamini C kiasi kidogo cha vitamin B Compleksi.

## TIP yaongeza uwezo wa ujasiriamali katika miradi ya kilimo

Mbali na TIP kuwa Wakala Mwezeshaji wa Programu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (*AMSDP*) kwa wilaya ya Arumeru, pia TIP imeteuliwa kuwa Wakala Mwezeshaji Kiongozi kwa wakala wengine. Kwa kushirikiana na CIAT shirika liliandaa mafunzo ya Undelezaji wa miradi ya kilimo kwa ajili ya wafanyakazi wake ofisi kuu na wa wilaya ya Arumeru. Mafunzo yalilenga njia za kutambua fursa za masoko kwa wakulima wadogo, na mikakati ya kuboresha ushindani wa mnyambuliko wa masoko kwa wakulima wadogo. Madhumuni makuu ya mafunzo haya ni kuiandaa TIP iwe na uwezo mkubwa zaidi wa kutoa mafunzo kwa wakala wenza 16 wa AMSDP wanaofanya kazi katika wilaya 20 zilizo katika mikoa 8.

Mafunzo haya ni kati ya mafunzo ambayo CIAT itatoa kwa wafanyakazi wa TIP. Shirika la CIAT liko Uganda na lina ushirikiano na TIP kwa miaka 4 sasa. Ni shirika linaloendeleza mbinu bunifu za ujasiriamali kwa wakulima wadogo kwa zaidi ya miaka 10, ambazo zimefanya kazi kwa mafanikio Amerika ya Kusini, Asia na Afrika.

**Maonyesho ya Kilimo Nane Nane**
Agusti 1-10, 2005
**Viwanja vya Themi, Arusha**

*Ujumbe*: Kilimo bora ni nyenzo muhimu ya kuondoa aina zote za umaskini

### Masoko hubadilika kutokana na mahitaji ya jamii za mijini

*Kutoka Uk. wa 1*

na kujenga mahusiano na wafanyabiashara.

Katika miji mingi mikubwa na midogo, kipato cha wakazi wake kimekuwa kikiongezeka. Kwa ongezoko la kimapato, watu hupenda kutumia kiasi kidogo cha mapato yao kwa ajili ya chakula. Pamoja na hayo walaji hupenda zaidi vyakula vilivyozalishwa katika mazingira ubora. Mazao yaliyozalishwa bila kutumia mbolea za viwandani na madawa makali ya kuulia wadudu, yamekuwa na nafasi kubwa katika masoko. Baadhi ya walaji wapo tayari kulipa gharama kubwa ili kupata vyakula vilivyozalishwa bila madawa.

Mahitaji makubwa ya vyakula kwa kuzingatia aina, ubora na wingi yapo mijini. Mahiitaji haya husaidia ongezeka la masoko ya kisasa (supermarkets). Ili kuweza kuuza bidhaa katika supamaketi wakulima hutakiwa kufikia kiwango kinachohitajika na soko hilo.

Kwingineko duniani, kumekuwa na matukio ya magonjwa na vifo vilivyosababishwa na vyakula vilivyo hifadhiwa vibaya. Kwa mfano, karanga ambazo zimepata uambukizo wa alfoltixin au kahawa yenye mycotoxin, vimejenga uelewa mkubwa wa utunzaji bora wa vyakula. Nchini Kenya, watu zaidi ya 100 walikufa kutokana na kula mahindi yaliyohifadhiwa vibaya mwaka 2004. Ubora wa mazao huhakikiwa wakati wa kupokelewa na wakati wa kutoka kwenye maghala ili kuhakikisha usalama wa chakula kwa jamii.

## W A T U

### Mfanyakazi wa Kujitolea kutoka Shirika la Visions in Action

Melanie Haske ni mfanyakazi wa kujitolea kutoka shirika lisilo ka kiserika la Visions in Action. Makao makuu ya shirika hili yako Washington D.C nchini Marekani. Amekulia maisha ya mji mdogo katika jimbo la Michigan. Anafurahi sana kuishi Moshi na amependezwa na ukarimu wa Watanzania. Atakuwa TIP kwa muda wa mwaka mmoja (kuanzia Jan-Des 2005). Ni mtaalamu wa ustawi wa taasisi na ataisaidia TIP katika shughuli za kuimarisha shirika. Shirika linafurahia huduma yake na juhudi zake.

### Wanafunzi wa chuo kikuu wilaya ya Arumeru

Kalista Maganga, Modesta John na Ronald Swai ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine. Wanafunzi hawa watakuwa TIP kwa wiki 5 kujifunza kazi kwa vitendo kuanzia Juni – Julai 2005. Kalista na Modesta watakuwa wakitathimini maendeleo ya shughuli za AMSDP katika eneo bonde la Nduruma na Ronald atafanya tathimini ya athari katika mazingira kwenye bonde la mto Kikuletwa.




Haki zote zimehifadhiwa, Mark Parisi

## Maswali Kuhusu Ukimwi

*Chanzo: UNICEF, **Majibu ukurasa 4.***
"VVU" – Virusi vya Ukimwi

1. Ukimwi ni:
   A. ugonjwa
   B. bakteria
   C. aina fulani ya madawa
5. Ukimwi huambukizwa kwa:
   A. virusi
   B. uharibifu wa mazingira
   C. vyoo vichafu
3. Kinga ya mwili inafanya kazi gani?
   A. Husaidia mwili kupambana na magonjwa, kama vile mafua,au homa ya mapafu
   B. Huongeza uwezo wa macho kuona
   C. Hujenga misuli imara
4. VVU, ni virusi ambavyo husababisha Ukimwi:
   A. vinaweza kuzuiliwa kwa chanjo
   B. vinaweza kuambukizwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine
   C. haviwezi kuambukizwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine
5. Pindi mtu apatapo uambukizi wa VVU, ni wakati huo huo hupata Ukimwi?
   A. Kweli
   B. Si kweli
6. Watu wote wenye ukimwi huonyesha dalili sawa:
   A. Kweli
   B. Si kweli
7. Dawa mpya imepatikana inayotibu ukimwi:
   A. Kweli
   B. Si kweli
8. Bila dawa za kurefusha maisha kwa mtu aliyeathirika, ukimwi humuua katika kipindi cha:
   A. miezi 6 mpaka miaka 2
   B. wiki 1 mpaka 2
   C. miaka 5 mpaka 10
9. VVU huambukizwa kwa:
   A. kukaa karibu na mtu aliyeathirika
   B. kumbeba mtu aliyeathirika
   C. kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mtu aliyeathirika bila kutumia kinga.
10. VVU huweza kuambukizwa kwa njia ya mbu:
   A. Kweli
   B. Si kweli

# Habari za wilayani

## Arumeru

### Hifadhi ya ardhi na maji na ongezeko la mazao

Mwaka 1997 TIP ilianza kufanya kazi na wakulima wa kikundi cha watumia maji Maroroi cha kata ya Nduruma. Mafunzo ya hifadhi ya ardhi na maji ni mojawapo ya shughuli zilizofanywa. Waliwezeshwa kufanya ziara ya mafunzo wilayani Lushoto. Baada ya kurudi, kikundi kiliunda kikundi cha mazingira ili kueneza ujuzi kwa wakulima wengine. Bw. Meivashi – Mwenyekiti wa mazingira wa kikundi, anasema, "kwa wakulima ambao wametumia mbinu za hifadhi ardhi na maji wamefaidika sana". Kuna upungufu mkubwa wa mmomonyoko wa udongo, kuna wingi wa majani kwa malisho ya mifugo, na kuna ongezeko kubwa la mavuno. Mavuno kwa ekari moja yalikuwa gunia 3-4 za mahindi kabla ya kuwezeshwa na TIP. Lakini sasa mavuno ni gunia 9-12 za mahindi na 4-5 za maharage kwa ekari.

### Kikundi kilichofanikiwa kuuza Jibini

IDAFASO ni kikundi kati ya vikundi 18 vilivyo chini ya Programu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (AMSDP) kilichopo kata ya Nkoaranga. Baada ya kupata mafunzo ya utafiti wa masoko na kilimo cha mkataba kutoka TIP, kikundi kimepata soko jipya la bidhaa zake. Kina mkataba wa kuuza jibini katika supamaketi ya Ndiyo na Hoteli ya Livingstone. Pia huuza kilo 10 za jibini kwenye hoteli ya ViaVia. Kikundi kimeimarika na kimefanikiwa kukuza uzalishaji na biashara ya bidhaa zake. Kinauza maziwa, siagi, jibini na maziwa mtindi.



Mrs. Massawe (left) with IDAFASO group in Arumeru district displays milk products. Second left is Manager of CIAT agro-enterprise development project, Shaun Ferris.

## Lushoto

### Ukarabati wa ndiva.

Kumalizika kwa ukarabati wa ndiva ya kikundi cha watumia maji cha Dule, kumewezesha kuboreka kwa maisha ya wakulima wa kikundi hicho. Uwezo wa kuhifadhi maji wa ndiva ya Dule umeongezeka kutoka mita za ujazo 5 - 70. Ongezeko la maji limesaidia kuwepo kwa uzalishaji katika kipindi chote cha mwaka na kusadia upatikanaji wa chakula na ongezeko la kipato. Eneo la umwagiliaji limeongezeka kutoka hekta 3 - 10. Uzalishaji umeongezeka kutoka magunia 4 – 8 ya viazi mviringo kwa robo eka kwa msimu. Matumizi ya maji yanayovunwa si kwa umwagiliaji tu bali hutumika pia kwa matumizi ya nyumbani.

## Mwanga

### Majirani waiga ujuzi.

Wakulima wa kikundi cha Kwa Mlombola wamefanikiwa kutoka katika mfumo wa kulima kwa ajili ya chakula na kulima kibiashara. Mabadiliko haya yametokana na kutumia mbinu bunifu kwenye uzalishaji na kukabiliana na masoko. Wakulima humwagilia kwa kutumia vinyunyizi mrashi visivyohitaji mgadamizo mkubwa na kwa njia ya matone kwa ajili ya kuongeza matumizi bora ya maji. Robo ekari iliyooteshwa nyanya au pilipili hoho humuingizia mkulima kiasi cha sh. 200,000/= kwa msimu. Kutokana na mafanikio ya kikundi cha Kwa Mlombola, baadhi ya wakulima kutoka ndani na nje ya vijiji vya jirani wameanza kuiga ili nao wafanikiwe. Mmoja wao ni Bw. Eliakim Mrutu ambaye anatumia mianzi kunywesha shamba lake lenye ekari 2 kwa njia ya matone.

### Wanawake wapata sauti sawa.

Kutokana na kuboreshwa kwa mifumo ya umwagiliaji, mtiririko wa maji kwenye kikundi cha Chunguli umeongezeka kutoka lita 18 – 120 kwa sekunde. Baada ya mafuzo ya uimarishaji wa vikundi na jinsia, wanawake sasa wana usawa katika kutumia maji ya umwagiliaji. Kabla ya hapo hapakuwa na mwanachama mwanamke kakika kikundi cha Chuguli, lakini sasa asilimia 45% ya wanachama ni wanawake. Eneo la kilimo limeongezeka kutoka ekari 15 mpaka 24. Zaidi ya hayo mafunzo ya kilimo bora yamesaidia ongezoko la uzalishaji.

## Same

### Kilimo cha tangawizi

Wakulima wa Mamba Myamba walipata habari ya mafanikio ya Chome kutoka TIP mwaka 1989. Baada ya kufanya ziara ya mafunzo Chome, waliamua kujenga matuta katika mashamba yao. Mwaka 1994, mkulima mmoja wa Mamba alitembelea Lushoto kwenye mashamba yanoyooteshwa tangawizi. Alirudi na mbegu na kuotesha katika matuta waliyotengeneza. Iliota kwa mafanikio sana na msimu uliofuata wakulima wengine waliamua kuotesha. Msaada Robson, mkulima wa Kikundi cha Watumia Maji cha Nongo alisema kuwa zao hili lina faida nyingi. Linafaa kuchanganywa na mazao mengine, lina soko ndani na nje ya nchi, na bei yake ni kati ya shilingi za Kitanzania 300 – 500 kwa kilo.

### Mafanikio ya zao la vitunguu.

Kabla ya TIP kuingia katika eneo bonde la Chome mwaka 1988, mazao ya biashara yalikuwa kahawa na miwa tu. Kwa sasa vitunguu ndio zao kuu la biashara. Wakulima wamehifadhi ardhi yao kwa njia ya matuta baada ya kupata elimu ya hifadhi ardhi na maji kutoka TIP. "Vitunguu vyetu ni bora kuliko vingine kutokana hali ya hewa na udongo wa eneo letu" alisema Richard Daniel mkulima wa Chome. Vitunguu huvunwa baada ya miezi mitatu au minne na kutoa nafasi kwa mazao mengine kuoteshwa. Richard alisema kuwa zao hili limesaidia kuongeza kipato katika familia na kuiwezesha jamii ya Chome kumudu kulipia ada za shule na kujenga nyumba.

TIP ni shirika lisilo la kiserikali la Uboreshaji Kilimo cha Umwagiliaji wa Mifereji Asili na Mazingira lililosajiliwa tangu mwaka 1999. Hata hivyo shirika hili lisilo la kiserikali lililoundwa mnamo mwaka 1988, wakati ambao TIP lilianzishwa kama Mpango wa Uboreshaji Mifereji ya Asili chini ya waasisi wa shirika la Maendeleo la Uholanzi (Netherlands SNV).

TIP inashirikiana na Halmashauri za Wilaya ili kuweza kuwafikia kwa urahisi walengwa ambao ni wakulima wa maeneo ya umwagiliaji kwa mifereji ya asili.

Malengo ya TIP ni kuboresha na kuinua viwango vya maisha ya jamii za maeneo ya Tanzania yenye ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia mifereji ya asili, kuhifadhi maji na udongo, kustawisha misitu na maeneo ya vyanzo vya maji nchini Tanzania.

TIP inalenga kuhudumia vikundi vidogo vya wakulima (me na ke) vilivyo katika maeneo yenye umwagiliaji Tanzania.

**Kifurushai cha TIP**

1. Uimarishaji wa vikundi na Jinsia
2. Ushirikishwa wa Matumizi bora ya ardhi
3. Uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji
4. Kuyakabili masoko na uendelezaji wa miradi ya kilimo

**SHUKRANI:**
**Shirika la TIP linapenda kutoa shukrani za pekee kwa:**
**NOVIB, UBALOZI WA JAPANI, UBALOZI WA UHOLANZI na SHIRIKA LA MAENDELEO LA UMOJA WA MATAIFA (UNDP) Kwa ufadhili wa shughuli za TIP**

**Tuandikie:**
Tuma maoni yako, mapendekezo, ushauri, hadithi na mawazo yako kwa kutumia anwani ya TIP, andika jina lako kamili na anwani yako

TIP
S.L.P. Box 8909, Moshi - Kilimanjaro
Simu : 027 53025 / 54232
Faksi: 027 51124

Barua pepe: tip@tiptz.org
Mtandao: www.tiptz.org




**Majibu ya Maswali ya Ukimwi**
Kutoka ukurasa wa 2

1. A. Maana ya UKIMWI ni "Upungufu wa Kinga Mwilini". Mtu mwenye Ukimwi hupungukiwa na kinga ya mwili.
2. A. Ukimwi husababishwa na Virusi vya Ukimwi (VVU). VVU hudhoofisha na kuua chembe hai za mfumo wa kinga mwilini. Mwili hushindwa kupambana na maambukizi ya magonjwa unapopata maambukizi ya VVU.
3. A. Mwili una mfumo wa kinga ambao hupambana na maambukizi ya magonjwa. Unapopata maambukizi, mfumo huzalisha chembe hai zinazopambana na maambukizi. VVU ni hatari kwa sababu hudhoofisha ama kuua mfumo wa kinga mwilini.
4. B. VVU huambukizwa kwa njia ya kuwekewa damu iliyokwisha athirika, kushirikiana vitu vyenye ncha kali (mfano nyembe,sindano n.k), kuwa na uhusinao wa kimapenzi bila kutumia kinga. Maambukizi hutokea kwa mtoto wakati wa kuzaliwa au wakati wa kunyonya. Kinga dhidi ya VVU haijapatikana.
5. Si kweli. Pindi mtu apatapo maambukizi ya VVU, hupata ukimwi kuanzia miezi 6 mpaka miaka 10 au zaidi.
6. Si kweli. VVU ni virusi vinavyosababisha Ukimwi, hudhoofisha na kuua nguvu ya mwili kujikinga na maradhi. Kwa hiyo mtu mwenye Ukimwi hupatwa na magonjwa ya aina mbalimbli na yenye dalili tofauti. Mojawapo ya dalili hizo ni kupoteza uzito.
7. Si kweli. Zipo dawa za kurefusha maisha lakini hazitibu ukimwi na gharama yake ni kubwa.
8. A. Mtu mwenye Ukimwi, hupoteza maisha baada ya kupata maambukizi ya magonjwa kutokana udhaifu wa kinga mwilini kuweza kupambana na magonjwa.
9. C. VVU husambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi bila kutumia kinga, kushirikiana vitu vyenye ncha kali (mfano nyembe, sindano) n.k.
10. Si kweli. Mbu hawezi kusambaza virusi vya ukimwi

## Shamba Mfano la TIP Moshi

Shirika la TIP limekuwa likitembelewa na wageni wa aina mbalimbali wakiwamo watafiti, wafadhili, maafisa wa serikali, wakulima n.k. kwa nia ya kujifunza, kuona mafanikio yake na linavyotekeleza kazi zake. Mpaka wakati huu shirika lina njia mbili za kuelezea mafanikio na taaluma yake kwa wageni; moja ni kewapeleka vijijini, nyengine ni kuandaa maonesho madogo katika ofisi yake. Maonesho ya ofisini hayatoi mvuto kama ambavyo wageni wangeona kazi halisi kule vijijini. Shirika limeamua kutengeneza shamba la mfano katika eneo la ofisi kuu. Katika shamba mfano kuna matuta ya mawe na matuta ya udongo yanayomwagiliwa kwa vinyunyizi mrashi. Lengo la kuwa na shamba mfano ni kwa kutoa mafunzo kwa wakulima walio karibu na kwa maonyesho.



**Mzee Kiwale akipalilia vitunguu katika shamba la mfano la TIP.**

## Pingamizi kwenye Juhudi zetu.

Katika kipindi cha miaka ya nyuma, kuliishi mfalme aliyeweka jiwe kubwa katikati ya moja ya barabara za milki yake. Baada ya kufanya hivyo alijificha na kuangalia kama kutatokea mtu yeyote atakayelitoa jiwe hilo. Baadhi ya wafanyabiashara wakubwa walipita kwa kulizunguka hilo jiwe. Wengi wao walimlaumu mfalme kwa kutotengeneza barabara za eneo lake. Pamoja na hayo, hakuna aliyeonyesha jitihada yoyote ya kuliondoa jiwe hilo. Baadaye alipita mkulima mdogo akiwa amebeba mboga. Alipofika kwenye jiwe, aliweka mzigo wake wa mboga chini na kuanza kuondoa jiwe aliloweka mfalme na kulisogeza pembezoni mwa barabara. Baada ya jitihada nyingi alifanikiwa kulisogeza. Aliponyanyanyua mzigo wake ili aendelee na safari yake, akaona pochi iliyokuwa imefichwa chini ya lile jiwe. Ndani ya pochi kulikuwa na vipande vya dhahabu na maelezo kuwa ni zawadi kutoka kwa mfalme kwa yeyote atakaye ondoa hilo jiwe barabarani. Mkulima alijifunza ni kitu gani ambacho wengi wetu hatuelewi. Kila pingamizi lililo mbele yetu hutoa fursa ya kuboresha hali zetu.

## Faida za kutofanikiwa

1. Kama hutafanikiwa, utagudua kisababishi.
2. Kutofanikiwa hutoa fursa ya kujaribu njia nyingine. *Roger Van Oech*